**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU RIPOTI YA HALI HALISI YA MAZINGIRA ZANZIBAR

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma, Muumba wa mgingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kufika hapa leo hii tukiwa katika hali ya uzima na amani na kuweza kutekeleza majukumu yetu ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, vile vile, nitumie fursa hii kukutakia heri na siha njema wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii mbele ya Baraza lako Tukufu kwa ajili kutoa maoni ya Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu uwasilishwaji wa **Ripoti ya Hali Halisi ya Mazingira Zanzibar.**

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa nafasi hii napenda kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya Salum kwa kuwasilisha kwa **Ripoti ya Hali Halisi ya Mazingira Zanzibar**. Ripoti hii inaonesha wazi jinsi Ofisi yake inavyotekeleza majukumu yake kwa kufuata taribu za kisheria.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa sasa naomba niwatambue kwa majina Wajumbe wa Kamati yangu kama ifuatavyo:

1. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Mwenyekiti

2. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Machano Ohman Said - Mjumbe
4. Mhe. Suleiman Makame Ali - Mjumbe
5. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Mjumbe
6. Mhe. Salma Mussa Bilal - Mjumbe
7. Mhe. Mohammed Mgaza Jecha - Mjumbe
8. Nd. Ali Alawy Ali - Katibu
9. Nd. Mwanaisha Mohammed Kheir - Katibu
10. Nd. Amina Abeid Hemed - Mkalimani wa Lugha za Alama

**Mheshmiwa Spika,** kwa dhati kabisa na kwa niaba ya Kamati hii napenda kuwapongeza viongozi wote wa Wizara hii pamoja na Taasisi zake zinazosimamia mazingira kwa kazi zao wanazozifanya zenye dhamira ya kuhakikisha mazingira yetu yanalindwa kwa nguvu zote na kwa mustakbali ya maisha ya sasa na vizazi vijavyo.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya utangulizi huo, sasa naomba kutoa maoni ya Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mnasaba wa **Ripoti ya Hali Halisi ya Mazingira Zanzibar** mbele ya Baraza lako tukufu kama ifuatavyo:

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali kupitia Taasisi zake zenye Mamlaka ya mazingira kutaja kwa ukamilifu eneo lote la bahari ya Zanzibar kwa kuzingatia mipaka ya pande zote nne yaani Kaskazini, Kusini, Mashariki na Magharibi mwa Zanzibar jambo ambalo litasaidia Mamlaka hizi kusimamia kikamilifu maeneo yote katika uhifadhi wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** katika *ukurasa wa 2* wa ripoti hii, Kamati imebaini kwamba muundo uliopo wa kuwa na Idara ya Mazingira na Mamlaka ya Mazingira ndani ya Wizara hii hauzko vizuri kiutendaji kwani Mamlaka ya Mazingira ndio yenye

nafasi kubwa katika masuala ya kiamzingira hivyo, iweze kupewa nguvu zaidi Mamlaka hii kama ilivyo kusudiwa. Aidha, Kamati inashauri Sheria ya Maizingira ya Mwaka 2015 kufanyiwa marekebisho yatakayoiwezesha Idara kutoa ripoti yake kila baada ya miaka miwili (02) tofauti na sasa ambapo hutolewa kila baada ya miaka mitano (05). Hata hivyo, Kamati imeona ni vyema kwa ripoti hii kutolewa na Mamlaka ya Mazingira badala ya kuandaliwa na kutolewa na Idara.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, Kamati inashauri Wizara hii kufanya jitihada za makusudi za kuitangaza siku ya mazingira kitaifa ili jamii iweze kufahamu juhudi zinazochukuliwa na Serikali kupitia Taasisi zake mbali mbali katika kupambana na suala la mazingira, jambo hili litasaidia jamii kuweza kushiriki kikamilifu katika kusimamia na kulinda mazingira katika matumizi endelevu.

**Mheshimiwa Spika,** Katika njia zilizotumika kukusanyia taarifa za ripoti hii ambazo zimeainishwa katika *ukurasa wa 3* wa ripoti hii. Kamati inashauri Idara ya Mazingira kutumia njia za kisasa ambazo zipo kitaalamu zaidi katika ukusanyaji wa taarifa za kimazingira na kuachana na njia za zamani ambazo kwa sasa zimeshapitiwa na wakati kama ambavyo wamtumia njia ya uzoefu kutoka nchi nyengine licha ya kwamba nchi hizo hazikutajwa katika ripoti hii. Vile vile, Kamati inashauri Idara ya Mazingira kwenda moja kwa moja katika malengo ya Ilani ya Chama Chama Mapinduzi yam waka 2020/2025 ambayo imefafanua vyema umuhimu wa jamii kuhifadhi mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** katika *ukurasa wa sita mpaka wa kumi* ambao umetaja Sera ya Kimazingira, Kamati imebaini kuwepo kwa Sera na Sheria nyingi za Mazingira ambazo zenyewe zinakinzana katika utekelezaji wa kazi zake, hivyo Kamati inashauri Serikali kufanya upya mapitio ya Sera na Sheria za Mazingira kwa kila Taasisi inayosimamia mazingira ili kuja Sera moja ambayo itakua rahisi katika utekelezaji wake. Hata hivyo, katika utekelezaji mzuri wa Sheria ya Mazingira ni

vyema jamii ikaeleimishwa vya kutosha kuhusiana na Sheria hii kwani wananchi wengi hawaifahamu ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba katika uingizwaji wa bidhaa ambazo hazina kiwango na salama katika matumizi ya binadamu zinaleta changamoto kubwa katika hatua zinazochukuliwa juu yake, ikiwa ni pamoja na kuteketezwa kwa bidhaa hizo. Hata hivyo, Kmati inashauri Sheria iweke adhabu ya muhusika anaeleta bidhaa ambayo haina kiwango au haifai kwa matumizi ya wanaadamu basi irejeshwe inakotoka badala ya kuteketezwa katika maeneo yan chi yet una hivyo kuleta uharibifu wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Ripoti ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ya Hali Halisi ya Maliasili Zisizorejesheka, Zanzibar ya Machi, 2019 ni kuwa Zanzibar ina jumla ya viwanda 37 vinavyojihusisha na uvunjaji wa mawe kwa ajili ya kupata kokoto na vumbi la kutengenezea matofali, pia idadi hiyo inaweza kuongezeka siku hadi siku. Kamati, inashauri Idara kuhakikisha wamiliki wa viwanda hivi wamehifadhi mazingira ipasavyo kwa kuyarudisha maeneo hayo katika hali ya kawaida lakini pia kuweza kulidhibiti vumbi linatoka katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati imebaini kwamba Zanzibar ina changamoto kubwa ya mpango wa Matumizi ya Ardhi, mpango ambao utaweka matumizi sahihi ya ardhi kwa mijini na vijijini. Kwa mfano maeneo yote ambayo yakitumia kwa shughuli za kilimo sasa yanatumika kwa makaazi ya watu bila kuwepo utaratibu maalum wa udhibiti wa maeneo hayo. Hali hii, imeathiri pia sehemu zenye vyanzo vya maji kama vile Mtopepo na Mwanyanya sehemu ambazo zilikuwa na vyanzo vikuu vya maji kwa mji wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Vile vile, Kamati imebaini kuwa kisima cha maji kiliopo eneo la Mwanakwerekwe 'C' hakipo salama kutokana na uharibifu mkubwa unaofanywa na watumiaji wa gereji iliyopo eneo hili. Aidha, Kamati inashauri

sehemu zote zenye vyanzo vya maji ambavyo zipo kwe nye makazi ya watu kulindwa kutokana na uharibifu wa mazingira kwa kujengewa vibanda na kuwekewa walinzi kama hatua ya kukabiliana na changamoto ya uharibifu wa maneo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa vivutio vikubwa vya utalii Zanzibar vinahusiana kwa kiasi kikubwa na mazingira asilia ambavyo ni pamoja na Mji Mkongwe wa Zanzibar ambao umo kwenye Urithi wa Dunia unaotambuliwa na UNESCO mwaka 2000, *ukurasa wa 17 – 19.* Kamati inashauri Mamlaka inayohusika kufikiria kupunguza msongomano wa watu katika maeneo ya Mji Mkongwe kwa utaratibu maalum wa kuingia na kufanya kazi katika maeneo haya. Vile vile, Kamati inashauri Mamlaka ifanye utafiti kwa watu wote wanaoishi Mji Mkongwe ili kufahamu wenye uwezo wa kuzikarabati nyumba zao na ambao hawana uwezo basi wahamishwe kwa kutafutiwa sehemu za kuishi ili kupunguza msongomano wa watu katika maeneo ya Mji Mkongwe.

**Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na janga la Mabadiliko ya Tabianchi njia mbali mbali zimekuwa zikishauriwa ili kupunguza madhara ya mabadiliko ya Tabianchi ikiwa ni pamoja na kuweka miongozo ya Sera na Sheria, kupanda miti na matumizi ya nishati mbadala. Hivyo, Kamati inashauri wananchi waelimishwe juu ya matumizi sahihi ya nishati mbadala pamoja na kuangalia hali halisi ya Maisha ya wananchi wetu katika matumizi ya nishati mbadala.

**Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyengine, Kamati imeridhishwa na mpango wa Serikali kuanzisha shughuli za utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia tangu mwaka 2017 kwa shughuli za ukusanyaji wa taarifa kwa njia ya Anga, nnia ya nchi kavu nan jia ya baharini. Kamati inashauri utafiti wa kina ufanyike katika kukabiliana na majanga yote ya kimazingira ambayo yatatokea baada ya kuanza harakati za uchimbaji wa mafuta na gesi hususani katika maeneo ya bahari ambayo athari yake inaeneo kwa haraka zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** pia, Ripoti hii kupitia *ukurasa wa 37 – 40* imeelezea uwepo wa taka hatarishi ambapo kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Zanzibar ya mwaka 2015, taka hatarishi zimejumuisha taka za hospitali, chuma chakavu, kemikali chakavu na bidhaa chakavu za umeme na elektroniki. Kamati imebaini kuwa mpaka wakati huu bado Idara haijaweka mikakati madhubuti ya kukabiliana na changamoto za taka hizi. Kamati inashauri Serikali ifanye mpango wa kujenga kiwanda cha kuchakaza taka zote ambazo imekuwa ni tatizo katika nchi yetu. Aidha, Idara izisimamie kwa nguvu zake zote bidhaa chakavu za umeme na elektroniki ambazo kwasasa imekuwa biashara kubwa inayoingia Zanzibar na imekuwa chanzo cha uharibifu wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia naomba kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini wakati wote ambao naiwasilisha hotuba hii, na pia nizidi kuwashukuru wajumbe wa Kamati yangu kwa mashirikiano yao makubwa waliyonipatia pamoja na kuwa na msimamo thabbit katika kazi zetu. Aidha, niwaombe wajumbe wa Baraza hili Tukufu kuisoma na kuifahamu vyema ripoti hii ili tuweze kutoa maoni na ushauri wa kina kuhusiana na taarifa zilizomo katika ripoti hii.

**Mheshimiwa Spika;** “Naomba Kuwasilisha.”

…………………………
(Hassan Khamis Hafidh)
Mwenyekiti,
Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,
**BARAZA LA WAWAKILISHI**
**ZANZIBAR**